

Unatakiwa Kufanya Nini?

Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa. Kumbuka kwamba hakuna majibu yasiyokuwa sahihi. Tafadhali tafakari kwa makini kuhusu maswali hayo na utoe maoni yako mwenyewe.

KISA CHA 1

Samira na rafiki yake mkubwa Yonah wamezozana sana. Baadaye, Samira alisambaza chapisho baya sana kumhusu Yonah kwenye mitandao ya kijamii. Baadaye usiku huo, Yonah anamtumia ujumbe wa maandishi na wanasameheana, lakini chapisho lake bado lipo mtandaoni.



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Samira afanye nini? Yonah afanye nini?

Baadhi ya mifano ni kama: Mtu fulani anaweza kuona chapisho hilo na kumripoti Samira kuwa ni mwonevu au atafsiri vibaya uhusiano kati yake na Yonah na kuhusu hisia zao. Huenda Yonah bado akaliona chapisho hilo kuwa ni la kuumiza. Inaonekana ni jambo zuri kwa Samira kuliondoa chapisho lake.



Je, unaweza kufikiria mfano halisi wa maisha wa kisa kama hiki?

Wanafunzi wanapaswa kutafakari kuhusu mifano waliyokutana nayo au kusikia huko nyuma. Kumbuka kwamba kusimulia mifano hii halisi ya maisha kunaweza kukawafanya wanafunzi wasijisikie huru. Waombe wasimulie mifano ya marafiki au watu wanaowajua (badala ya wao wenyewe).

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Unatakiwa Kufanya Nini?

KISA CHA 2

Hiwot aliwapiga picha baadhi ya marafiki zake wakifanya mambo ya upuuzi kisha akazichapisha kwenye mitandao ya kijamii, pamoja na alama za reli zinazoonekana kuwa za kifidhuli au zenye kudhalilisha, lakini ilikuwa ni katika hali ya utani kati yake na marafiki zake. Katika siku iliyofuata, Nyawira, rafiki yake mwingine, alikuja shuleni kwake na kusema alifikiri kwamba alama hizo za reli ziliumiza sana na zilionesha ubaguzi wa kijinsia (yaani, ubaguzi unaojikita katika jinsia, hasa ubaguzi dhidi ya wanawake).



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Hiwot afanye nini? Nyawira anaweza kufanya nini kingine?

Hiwot anapaswa kuomba msamaha au ajieleze. Wanafunzi wanapaswa kufikiria jinsi watu wengine wanavyoweza kuelewa vibaya vitendo vyao tofauti na vile walivyokusudia, lakini hilo halimaanishi kwamba maoni ya watu wengine hayana maana.



Ingekuwaje kama Nyawira angekabiliana na Hiwot mtandaoni badala ya ana kwa ana?

Kama Nyawira angekabiliana na Hiwot kwenye chapisho hilo la umma, wengine wangeweza kutoa maoni kuhusu suala hilo na kueleza utani wa marafiki hao au kwa nini kauli hiyo ilikuwa ya kuudhi. Huenda hali hiyo ikasuluhishwa au ikawa mabishano makubwa miongoni mwa watu wengine wengi. Kama Nyawira angewasiliana na Hiwot kupitia ujumbe wa mtandaoni, basi Hiwot angeweza kuzungumza naye na kuhariri chapisho lake iwapo angeridhishwa kuwa halifai.

KISA CHA 3

Abigail alikuwa kwenye mitandao ya kijamii alipogundua kwamba Selam, mvulana shuleni, amempiga picha na kuandika, "Haha #whatnottowear" (akiyakejeli mavazi yake). Bila shaka Abigail alikasirika sana.



Ni nini kinachoweza kutokea? _____



Je, Selam afanye nini? Je, Abigail afanye nini?

Abigail anapaswa kukabiliana na Selam kuhusu matendo yake ili kumjulisha kwamba yalimumiza. Abigail anaweza pia kuripoti matendo ya Selam kwenye jukwaa la mtandao huo wa kijamii na kwa mtu mzima (kwa mfano, mzazi/mlezi, mwalimu au mkuu wa shule).

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.